



**KIAMBATA NAMBARI 3 KWA KIJITABU CHA TAARIFA KWA WAOMBAJI WA
USALAMA WA KIMATAIFA (IPO 1)**

NOTISI YA TAARIFA

**Taarifa inayohusiana na uamuzi wa Waziri wa kukubali au kukataa kutoa ruhusa ya
kubaki katika Nchi (Ayalandi)**

Chini ya kifungu cha 49(3) cha Sheria ya Ulinzi wa Kimataifa ya mwaka wa 2015, *katika kuamua kumpa au kutompa ruhusa mwombaji (ya kubaki katika Nchi), Waziri atazingatia familia ya mwombaji na hali yake ya kibinafsi na haki yake ya kuheshimu maisha yake ya kibinafsi na ya familia, kwa kuzingatia—*

- (a) aina ya uhusiano kati ya mwombaji na serikali, ikiwa ipo,*
- (b) maswala ya kibinadamu,*
- (c) tabia na mwenendo wa mwombaji wa ndani na (inapofaa na kuweza kuthibitishwa) nje ya Nchi (pamoja na hatia yoyote ya jinai),*
- (d) mazingatio ya usalama wa taifa na utaratibu wa umma,
na*
- (e) mazingatio yoyote ya faida ya kila mmoja.*

Kumbuka

Ingawa kwa kawaida Waziri ataweza kupata maelezo ya hatia za uhalifu zilizorekodiwa dhidi ya waombaji katika Nchi, ikumbukwe kwamba waombaji pia wanapaswa kutoa taarifa kwa Waziri kuhusiana na hatia yoyote ya jinai iliyorekodiwa dhidi yao ndani na nje ya Nchi.

**Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa
Agosti 2019**